

SHULE YA MSINGI YA TRENT PARK



Makubaliano ya Shule - Familia

FURSA ZA USHIRIKISHAJI WA MZAZI/FAMILIA

- Jiunge nasi kwa matukio ya Mpango wa Title I
- Jiunge na Baraza letu la Ushauri la Wazazi (PAC)
- Fanya kazi ya kujitolea madarasani na nyumbani
- Jiunge na darasa la mtoto wako kwenye safari ya kielimu
- Saidia tabia chanya kupitia sherehe shuleni

MATUKIO YA MPANGO WA TITLE I

Mkutano wa Msimu wa Mapukutiko - Wakati wa mkutano huu, unaofanyika Septemba au Oktoba ya kila mwaka, data ya shule hushirikiwa na familia. Pia tunaelezea maana ya kuwa shule ya mpango wa Title I, jinsi fedha zinavyotumika, na njia ambazo familia zinaweza kushirikiana na shule.

Usiku wa Kusoma - Wanafunzi hutumia muda pamoja na familia na walimu wao wakifurahia shughuli za kusoma. Tukio hili hufanyika Novemba au Desemba.

Usiku wa Hisabati - Wakati wa tukio hili, wanafunzi hutumia muda pamoja na familia na walimu wao wakitumia hisabati katika hali halisi. Jiunge nasi katika moja ya maduka ya vyakula mjini. Tukio hili litafanyika Januari.

Usiku wa Sayansi - Wanafunzi na familia zao hushiriki katika majaribio halisi mbalimbali ya sayansi. Tunafanya Usiku wetu wa Sayansi pamoja na Tamasha la Sayansi la NC mwezi Aprili.

Mkutano wa Msimu wa Machipuko - Taarifa Muhimu za mpango wa Title I zinashirikiwa na familia. Baada ya mkutano wa utangulizi, wanafunzi na wazazi hupata muhtasari wa mapema wa mambo ya kutarajia katika gredi inayofuata. Mkutano huu unafanyika Mei.

BARAZA LA USHAURI LA WAZAZI

Baraza letu la Ushauri la Wazazi (PAC) ni kundi la wazazi wanaoshirikiana na wafanyakazi wetu ili kuifanya Trent Park kuwa mahali pazuri pa kujifunza. Tunakutana mara kwa mara mwaka mzima ili kukagua na kurekebisha Mpango wetu wa Title I na Makubaliano, pamoja na kupanga matukio na kufanya maamuzi yanayoathiri shule yetu. Ikiwa una nia ya kujiunga na Baraza la Ushauri la Wazazi, tafadhali jaza fomu ya kuvutiwa katika anwani ifuatayo: bit.ly/3Zz6hXA (zingatia herufi kubwa na ndogo).

MAWASILIANO

- Ripoti za Maendeleo kila baada ya wiki 4½
- Kadi za Ripoti kila baada ya wiki 9
- Barua za mCLASS Home Connect kila baada ya wiki 9
- Alama za Mwisho wa Gredi (EOG) na Tathmini za Uchunguzi za North Carolina
- Mikutano ya wazazi
- Vipeperushi vya matukio
- Tovuti ya Shule, Facebook, Class Dojo
- Yanatolewa kwa lugha za Kiarabu, Kiburma, Kikareni, Kihispania, na Kiswahili zinapopatikana

AHADI ZETU

KAMA FAMILIA TUNAAHIDI...

- kusoma na kujadili kitabu cha mwongozo cha mwanafunzi cha TPE/CCS na mwongozo wa sera wa CCS pamoja na mtoto wangu.
- kupitia kazi ya mtoto wangu na kujadili maendeleo pamoja na mtoto wangu na mwalimu wake kwa kuhudhuria mikutano na kuwasiliana na shule.
- kuhudhuria matukio ya shule.
- kuhakikisha mtoto wangu anapumzika vizuri na anahudhuria shule mara kwa mara, na kupunguza mara za kuchelewa na kuondoka shuleni kabla ya wakati.
- kuzingatia matarajio makubwa ya kufuata kanuni na kuonyesha heshima.
- kusaini na kurudisha taarifa siku inayofuata au kama ilivyoombwa.
- kufuatilia kikamilifu shughuli za mtoto wangu mtandaoni na historia ya kuvinjari ili kuhakikisha matumizi yenye uwajibikaji na salama.
- kumhimiza mtoto wangu ajisomee yeye mwenyewe na anisomee pia.

KAMA MWANAFUNZI NAAHIDI...

- kuhudhuria shule kila siku na kwa wakati.
- kusoma na kujadili kitabu cha mwongozo cha wanafunzi cha TPE na familia yangu.
- kufuata kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi.
- kufanya kazi kwa bidii niwezavyo katika kazi zangu za shule.
- kumuuliza mwalimu wangu maswali wakati sielewi kitu.
- kujadili na familia yangu kile ninachojifunza shuleni.
- kutumia teknolojia ipasavyo na kwa usalama.
- kusoma angalau dakika 20 kila siku.

KAMA MWALIMU NAAHIDI...

- kuelezea matarajio yangu, malengo ya kufundishia, na mfumo wa kutoa alama kwa wanafunzi wangu na familia zao.
- kuelezea na kuimarisha kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi kwa wanafunzi na familia.
- kutoa mafundisho madhubuti na yanayofaa kulingana na viwango.
- kutoa uzoefu wa kujifunza unaovutia na unaotia moyo darasani mwangu.
- kutoa fursa za ushirikishaji wa wazazi, ikiwa ni pamoja na fursa za kufanya kazi ya kujitolea.
- kushirikiana na wazazi kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo ya wanafunzi, kushughulikia matatizo mapema, na kupanga mikutano inavyohitajika.

WASILIANA NASI

2500 Educational Drive, New Bern, NC 28562
Simu: (252) 514-6481
Faksi: (252) 514-6485
www.cravenk12.org/TPE

